

KISWAHILI NA MAENDELEO YA DINI

MICHAKATO MIPYA YA KUENEZA DINI KIUTANDAWAZI NA ATHARI ZAKE
KATIKA MUSTAKABALI WA MAENEZI YA KISWAHILI

Alex Umbima Kevogo
Chuo Kikuu Kishiriki cha Garissa
umbima2000@gmail.com

Mwenda Mukuthuria
Chuo Kikuu cha Mount Kenya
mukuthuria.mwenda@gmail.com

Dkt. Ayub Mukhwana
Chuo Kikuu cha Nairobi
ayubmukhwana@yahoo.com

Ikisiri

Kuna uhusiano baina ya kuenea kwa dini na kuenea kwa lugha. Kuenea kwa dhehebu la Kikatoliki na madhehubu mengine ya Kiprotestanti kulifanikisha kuenea kwa Kispanyola na Kiingereza katika maeneo ya Marekani Kusini, Afrika na hata Asia. Uhusiano wa lugha na dini hujitokeza wazi kiisimu ikizingatiwa kwamba lugha ni nyenzo ya kuenea dini. Aidha, kidini ni wazi kuwa asili ya lugha na dini aghalabu huchukuliwa kuwa na uhusiano ndiposa dini kuu za ulimwengu huhusishwa na lugha mahsusi za ulimwengu. Kuenea huku kunathibitisha uhusiano uliopo baina ya kuenea kwa dini na kuenea kwa lugha. Nchini Kenya, na hata Afrika Mashariki, hali hii inaweza kuthibitishwa kwa upande wa kuenea kwa dini ya Kikristo ambayo imefanikisha kuenea kwa Kiswahili hata katika maeneo ya mashinani ambako lugha hii haikuwa na wafuasi wengi. Majilio ya utandawazi yamewalazimu wahubiri kubuni na kufaragua mbinu mpya za kuenea injili katika maeneo yote yakiwemo yale ambayo hayakuzingatiwa awali. Hivyo, makala hii inalenga kudadisi mabadiliko ya miktadha ya kiutandawazi ya kuenea dini na athari za michakato hii mipya katika mustakabali wa maenezi ya lugha ya Kiswahili kipindi hiki cha utandawazi.